

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI MHESHIMIWA ENG.
EVARIST NDIKILO KATIKA HAFLA YA KUWAAPISHA WAKUU
WA WILAYA WAPYA WA MKOA WA PWANI**

TAREHE 01/07/2016

*Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa,
Katibu Tawala Mkoa,
Wakuu wa Wilaya Wateule,
Katibu wa CCM Mkoa,
Kamati ya Ulinzi na Usalama,
Makatibu Tawala wa Wilaya,
Wenyeviti wa Halmashauri za Mji na Wilaya,
Wakurugenzi wa Miji na Halmashauri za Wilaya,
Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo
Sekretarieti ya Mkoa,
Viongozi wa Dini,
Viongozi wa Taasisi mbalimbali,
Watumishi wote katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
Waandishi wa Habari,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.*

Ndugu zangu;

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai hadi leo hii tunapokutana katika hafla hii muhimu. Aidha, nitumie fursa hii kuwakaribisheni nyote hapa Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Pwani.

Ndugu Viongozi na Watumishi;

Leo ni siku maalumu kwetu sote katika Mkoa wetu wa Pwani. Ni siku ambayo tunawapokea na kushuhudia kuapishwa kwa Wakuu wa Wilaya wapya ambao wameteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa niaba ya Viongozi na Wananchi wa Mkoa wa Pwani napenda kuwapongeza sana Wakuu wa Wilaya mlioteuliwa ambapo Mheshimiwa Rais ameonyesha imani kubwa kwenu na kuwateua kuwa wawakilishi wake kwenye ngazi za Wilaya.

Nawapongeza sana kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi za Mkuu wa Wilaya. Ni shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais lakini pia ni shukrani kubwa kwa Mwenyezi Mungu. Hasa ukizingatia kwamba nchi yetu ina Watanzania wengi wenye sifa za kuwa Wakuu wa Wilaya, wanayo elimu ya kutosha, ni vijana, wachapakazi, lakini bahati imewaangukia ninyi.

Ndugu zangu, Viongozi na Watumishi;

Tunapowapokea viongozi wenzetu wanaoungana nasi katika kuwatumikia Wananchi wa Mkoa wa Pwani, tunao wajibu mkubwa wa kutumia fursa hii iliyotuleta pamoja kutafakari juu ya mafanikio tuliyoyapata na changamoto zilizopo mbele yetu ili kwa umoja wetu tuone namna ya

kudumisha mafanikio yaliyopatikana na kuweka mikakati ya namna ya kukabiliana na changamoto zilizopo mbele yetu.

Ndugu zangu, Viongozi na Watumishi;

Wakuu wa Wilaya niliowaapisha leo, wanaendelea kufungua ukurasa mpya kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa na nchi yetu kwa ujumla. Yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Mkoa wetu kwa uongozi wa awamu zilizopita. Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 - 2020 ndiyo itakuwa Dira Kuu itakayotuongoza wote katika kutekeleza mambo mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika awamu zilizopita tumesimamia na kutekeleza vizuri maelekezo na maagizo mbalimbali ya Kitaifa na Kisekta hususan Elimu, Afya, Maji, Kilimo, Ujenzi wa Barabara, Umeme, Ukusanyaji wa Mapato, Uwekezaji na Ajira kwa Vijana n.k. Kuhusu ulinzi na Usalama, hali ya Mkoa imeendelea kuwa shwari ukiachilia mbali vurugu chache za hapa na pale.

Pamoja na mafanikio katika sekta nilizozitaja hapo juu, Mkoa bado una mambo kadhaa ya kuyashughulikia ili kujiletea maendeleo. Taarifa ya kila Wilaya imeandaliwa ambayo kila mmoja wenu amepewa ili imsaidie kuanza kutatua changamoto mbalimbali zilizopo. Hata hivyo yapo maagizo ya jumla ambayo yanamhusu kila Mkuu wa Wilaya ambayo anatakiwa kwenda kuyasimamia ipasavyo: Maagizo hayo ni kama haya yafuatayo:-

- (i) Mkiwa Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, hakikisheni mnalinda amani na utulivu katika wilaya zenu ili wananchi wapate fursa ya kujishughulisha na kazi za maendeleo ili wapate vipato na kupunguza umaskini. Pambaneni na

uhalifu wa aina zote mfano; madawa ya kulevya, ujambazi wa kutumia silaha, mauaji ya albino, n.k. mjue kwamba changamoto za uhalifu zinazotokea Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Mtwara zinaweza kutokea katika Mkoa wetu. Mikoa yetu iliyoko Kanda ya Mashariki ina changamoto zinazofanana.

Masuala ya kihalifu yaliyoutikisa Mkoa wetu wa Pwani katika maeneo ya Ikwiriri, Mkuranga, Mafia, Kongowe nataka yasijrudie tena. Ni aibu kwa askari aliyepewa mafunzo ya kijeshi tena mwenye silaha kuvamiwa, kunyang'anywa silaha na kuuawa.

- (ii) Wasikilizeni wananchi, sikilizeni kero zao na malalamiko yao ili myatatue kwa wakati. Nendeni vijijini, mzungumze nao na msikilize changamoto zao. Haipendezi wananchi wafike Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili waeleze malalamiko yao wakati kuna Serikali ya Kijiji, Watendaji wa Vijiji na Kata, Afisa Tarafa, Mkurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wake na Mkuu wa Wilaya.

Mjue/tambueni kwamba bila kuwepo wananchi, hakuna Mkuu wa Wilaya wala Mkuu wa Mkoa.

- (iii) Zisimamieni Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri zenu) ili ziwatumikie wananchi. Halmashauri hizi zinapewa fedha nyingi hivyo ni lazima zitoe huduma bora kwa wananchi.

- Simamieni Raslimali Fedha na Raslimali Watu katika Halmashauri zenu. Kwa mfano; ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri - Mafia (Uvuvi), Kibaha (Soko, Stendi ya Mabasi, mchanga, viwanja, n.k).
- Watumishi wa Halmashauri waachane na kufanya siasa katika kutekeleza majukumu yao.

(iv) **Shughuli za Kilimo:** Kilimo ndiyo uti wa mgogo wa uchumi wa watu wetu. Kilimo ndicho kinachoajiri watu wengi zaidi mkoani kwetu na taifa kwa ujumla kuliko sekta nyingine.

- Zao la biashara litokanalo na kilimo cha korosho ni la muhimu kusimamiwa katika wilaya zenu. Kwa mfano, katika msimu uliopita 2015/2016, wakulima waliweza kuuza korosho zenye thamani ya shilingi bilioni 18.2. Kwa hiyo nawataka mkalisimamie zao hili la korosho katika palizi, kupulizia dawa mikorosho, upandaji wa miche mipya ya mikorosho, upatikanaji wa pembejeo kwa wakati n.k.
- Msicheke na Maafisa Kilimo wa Wilaya au Kata wanaofunga tai na kukaa ofisini wakati mashamba ya mikorosho yamefunikwa na nyasi.

- Simamieni maazimio yaliyotolewa na wadau wa korosho katika mkutano uliofanyika Mkuranga mwezi Mei, 2016.
- (v) Tumedhamiria kuufanya Mkoa wa Pwani uwe ni ukanda wa uwekezaji na hususan Viwanda (Industrial zone). Fursa hiyo tunayo kwa sababu ya ardhi kubwa iliyopo, soko karibu na Dar es Salaam, Barabara za lami kwenda kwenye masoko ya mikoa mingine na nje ya nchi, Reli ya Kati na TAZARA, Bandari, Uwanja wa Ndege upo karibu, n.k.
- Hakikisheni mnakuwa siyo kikwazo cha Wawekezaji ama Wasaidizi wenu wanaoendeleza urasimu usiokuwa na Tija ambao unakimbiza/unazuia uwekezaji.
 - Kumbukeni Agizo la Rais la kuvutia wawekezaji ili nchi yetu iwe ya uchumi wa viwanda.

Jitihada kadhaa zimefanyika kuvutia uwekezaji Mkoani kwetu, bado jitihada zaidi zinatakiwa kufanyika ili Wawekezaji waone Mkoa wetu ni mahali salama na muafaka pa kuwekeza ikiwemo kujenga viwanda mbalimbali ili kuufanya Mkoa wetu uwe Mkoa wa viwanda. Maeneo mahsusi ya kufanyia kazi ni kutenga na kupima maeneo kwa ajili ya Uwekezaji kwenye Kilimo na Viwanda. Aidha, miundombinu muhimu kama barabara, umeme na maji vipelekwe kwenye maeneo hayo.

Urasimu usiyo wa lazima, kuchelewesha vibali vya ujenzi na mengineyo visiwepo kabisa.

- (vi) Simamieni uundwaji wa Kamati za Amani katika Wilaya zenu ili zisaidiane na Kamati ya Amani ya Mkoa ambayo inaundwa na Wajumbe kutoka Dini ya Kikristo na Dini ya Kiislamu. Hili ni Agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kila Mkoa ni lazima uwe na Kamati ya amani ili isaidiane na Serikali ya Mkoa katika kulinda amani na utulivu wa wananchi. Viongozi wa dini ni watu muhimu katika amani ya nchi yetu. Mkitumia Kamati hizi, Viongozi wa Dini watawasaidia kujua viashiria vyote vya uvunjifu wa amani vinavyotokana na imani za Dini. Aidha, wahalifu katika jamii wanafahamika na wengine wanasali katika nyumba za Ibada, hivyo viongozi wa Dini watakuwa ni msaada mkubwa katika kulinda amani katika jamii.
- (vii) Hakikisheni Halmashauri zinatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015 kipengele kwa kipengele. Serikali ya awamu ya 5 ni ya Chama cha Mapinduzi.
- Vyama vilinadi Ilani zao na Ilani ya CCM ndiyo ilichaguliwa na wananchi katika uchaguzi wa Oktoba 2015.
 - Ilani ni Mkataba kati ya CCM na Wananchi kwa miaka 5 ijayo.
 - CCM iliunda Serikali ili itekeleze Ilani yake.

- Wakuu wa wilaya hakikisheni Ilani hiyo inatekelezwa kwa asimilia 100.

(viii) Simamieni na mtatue migogoro ya ardhi iliyopo katika Wilaya zenu kwa uwezo wenu wote, na kwa nguvu zenu zote. Migogoro hiyo ni ile baina ya wakulima na wafugaji, baina ya wananchi kugombania viwanja, na wananchi kuvamia mashamba. Migogoro ikiachwa bila kushughulikiwa inaweza kusababisha uvunjifu wa amani, mapigano, na kusababisha uharibifu wa mali na wakati mwingine watu kupoteza maisha. Tusirudie kuona mapigano kama yaliyotokea Ikwiriri Rufiji baina ya wakulima na wafugaji.

Taarifa zilizopo ni kwamba Mkoa una migogoro ya ardhi ipatayo 47 (Mkuranga 6, Kisarawe 7, Bagamoyo 7, Kibaha Vijijini 7, Rufiji 9, Mafia 5 na Kibaha Mji 6). Migogoro hiyo inahusiana na uvamizi wa mashamba yanayomilikiwa kisheria, uvamizi wa maeneo ya Serikali, migogoro ya wakulima na wafugaji n.k. Natoa wito kwa wale wote wanaomiliki mashamba makubwa wayaendeleze na wasiyaache mapori. Kwa ujumla jitihada za makusudi zinatakiwa ili kupunguza au kuondoa kabisa migogoro hiyo.

(ix) Wastani wa Pato la Mwananchi wa Mkoa wa Pwani kwa mwaka ni shilingi 1,253,378/=. Pato hili lipo chini ukilinganisha na mikoa mingine ya Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Arusha na Iringa. Aidha, mchango wa Mkoa wetu kwenye pato la

Taifa ni 1.81% tu wakati tunazo fursa na raslimali nyingi ambazo zinaweza kuongeza wastani wa pato la mwananchi na pia tukawa na mchango mkubwa wa Mkoa wetu kwenye pato la Taifa. Wakuu wa Wilaya hakikisheni kwamba katika kipindi cha miaka 5 ijayo mkoa wetu ni lazima uwe na ongezeko la wastani wa pato la mwananchi hadi 1,500,000/= kwa kuzitumia kikamilifu fursa zilizopo za uwekezaji, kilimo, biashara, uvuvi, uwezeshaji wananchi n.k.

- (x) Lipo wimbi kubwa la uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya mbao, mkaa na magogo katika Mkoa wetu. Hili linakwenda sambamba na uvamizi kwenye maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli nyingine za kibinadamu kama kilimo na ujenzi wa makazi. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya kuhakikisha uharibifu wa mazingira unakomeshwa haraka iwezekanavyo.
- (xi) Uhamiaji Haramu ni tatizo katika Mkoa wetu kwa kuwa ni mapitio ya wahamiaji hao kutoka nchi za Ethiopia, Somalia na Kenya kwenda nchi za Msumbiji, Afrika Kusini na Zambia. Bandari bubu za Bagamoyo ndiyo maingilio makuu. Pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, bado suala hili ni tatizo. Nawasihi wenzangu tuendeleo kufanya jitihada za makusudi kukabiliana na changamoto hii. Ulinzi shirikishi unapaswa kuhimizwa katika ngazi zote.

- (xii) Mmekabidhiwa Taarifa ya Hali Halisi ya Mkoa wa Pwani pamoja na Maelekezo ya Kiutendaji wa kila Mkuu wa Wilaya. Maelekezo hayo ni mahsusi (specific) kwa kila Mkuu wa Wilaya katika eneo lake la utawala.

Ninawataka musome taarifa hizo kwa makini ili baadaye nitapenda kupata Mpango Kazi wa kila Mkuu wa Wilaya alivyojipanga kutekeleza hayo maelekezo ya kiutendaji. Wataalamu wa Sekretarieti ya Mkoa wamefanya kazi nzuri ya kuandaa changamoto za kila Wilaya.

Ndugu Viongozi na Watumishi,

Maeneo yaliyotajwa hapo juu yana changamoto zake. Wajibu wetu ni kila mmoja kwenye eneo lake afanye kazi kwa bidii na kwa ubunifu na kwa kuzingatia Falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya HAPA KAZI TU!. Matarajio yangu ni kuona kwamba changamoto zinazojitokeza zinafanyiwa kazi ili tuboreshe huduma kwa wananchi na kuleta maendeleo ya taifa letu.

Ndugu Viongozi, Watumishi na Wageni Waalikwa,

Nimalize hotuba yangu kwa kuwasihi kila Mkuu wa Wilaya kwenye eneo lake akatekeleze majukumu yake kwa uadilifu mkubwa, changamoto zilizopo zikiwa ndiyo dira ili tuweze kuzitatua. Aidha, kila Mkuu wa Wilaya amekabidhiwa Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 na Taarifa fupi ya hali ya Wilaya ili kuwaongoza, pamoja na mambo mengine katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Ni matumaini yangu makubwa mkitekeleza majukumu mkiwa pia na **HOFU** ya Mungu mtafanikiwa.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**EVARIST W. NDIKILO
MKUU WA MKOA WA PWANI**

01 JULAI, 2016